TOLEO MAALUM KWA AJILI YA WANANCHI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA 2011/12

YALIYOMO

DIBAJI V

SURA YA KWANZA 1

1.0 UTANGULIZI 1

1.1 MAJUKUMU YA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI 1

1.2 RASILIMALI ZA TAIFA (UMMA) 2

1.3 MAANA YA UWAJIBIKAJI 2

SURA YA PILI 5

2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI 5

2.1 HATI ZA UKAGUZI 5

SURA YA TATU 10

3.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU 10

3.1 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA RIPOTI ZA UKAGUZI WA SERIKALI KUU KWA MIAKA YA NYUMA 10

3.2 MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA 11

3.3 MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2011/2012 12

SURA YA NNE 16

4.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA 16

4.1 HOJA ZA HALMASHAURI ZA MIAKA YA NYUMA ZISIZOJIBIWA 16

4.2 MWELEKEO WA JUMLA WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 16

4.3 MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA HESABU ZA HALMASHAURI KWA MWAKA 2011/2012 20

4.4 MATOKEO YA KAGUZI MAALUM 26

SURA YA TANO 28

5.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA 28

5.1 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA RIPOTI ZA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MIAKA YA NYUMA 28

5.2 UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012 30

5.3 HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA MASHIRIKA YA UMMA 30

5.4 MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA HESABU ZA MWAKA 2011/2012 31

SURA YA SITA 41

6.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO 41

6.1 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA RIPOTI ZA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MIAKA YA NYUMA 41

6.2 MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA 43

6.3 MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA HESABU ZA MWAKA 2011/2012. 44

SURA YA SABA 58

7.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA UFANISI NA UKAGUZI MAALUM 58

7.1 USIMAMIZI WA UKAGUZI WA MAGARI NA UKOMO WA MWENDO BARABARANI 59

7.2 UKAGUZI WA USIMAMIZI WA USALAMA MAHALI PA KAZI 63

7.3 USIMAMIZI WA MIKATABA YA MIRADI YA UJENZI KATIKA SERIKALI ZA MITAA 65

7.4 USIMAMIZI WA MANUNUZI YA VIFAA VYA TEHAMA KATIKA SEKTA YA UMMA 68

7.5 USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA ZIWA VICTORIA 70

SURA YA NANE 75

8.0 UJUMBE KWA WADAU WOTE WA RIPOTI HII 75

DIBAJI

Wananchi na jamii kwa ujumla wanayo haki ya Kikatiba kupata taarifa sahihi za Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mipango na miradi mbalimbali ya maendeleo kupitia vyombo vya habari na njia nyingine za mawasiliano. Kutokana na ongezeko la matumizi ya ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa vyombo vya habari na wadau wengine, kumekuwa na upotoshaji mkubwa wa taarifa za ukaguzi kwa namna zinavyotumiwa na wadau mbalimbali.

Ili kupunguza upotoshaji na kufanikisha mjadala wa masuala ya taarifa za ukaguzi nimeona nifanye jitihada za kuelimisha umma wa Watanzania ili uweze kuelewa na kuchambua masuala ya ukaguzi kwa usahihi kulingana na mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu. Jitihada hizo ni pamoja na kuandaa kitabu kidogo kinachoelezea muhtasari wa ripoti hizo kwa lugha rahisi na rafiki itakayosaidia kufikisha ujumbe sahihi kwa jamii.

Kwa mara ya kwanza Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) imeandaa kitabu hiki ambacho ni muhtasari wa ripoti zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zilizowasilishwa kwa Mhe. Rais na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi imeandaa muhtsari (kijitabu maalum) kinachoainisha masuala muhimu yaliyojitokeza kwenye ukaguzi ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Ripoti za ukaguzi wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2012 ziliwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 29 Machi, 2013 na baadaye kusomwa bungeni na

Mawaziri husika tarehe 11 Aprili, 2013. Ripoti hizi ziliwasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu Na. 34(1)(c) cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008.

Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 imeongeza mawanda ya ukaguzi kwa kuongeza madaraka ya kufanya kaguzi nyingine zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha. Kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria hii CAG anatakiwa kufanya ukaguzi wa ufanisi, utambuzi, mazingira na kaguzi mbalimbali maalum kama zitakavyojitokeza. Uhuru wa kiutendaji wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa kiasi kikubwa umeimarika baada ya kuanza kutumia sheria ya ukaguzi wa umma Na. 11 ya mwaka 2008. Hata hivyo, kulingana na viwango vya kimataifa maboresho zaidi yanahitajika hasa kwa upande wa kupanga mishahara na ajira za watumishi wa ofisi hii ili kuiwezesha kutekeleza majukumu ya kikatiba kwa ufanisi zaidi.

Ingawa majukumu ya ofisi ya CAG na yale ya taasisi za umma yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora wa rasilimali za taifa (Umma) yanafanana. Ni matumaini yangu kwamba, kwa kutumia sheria ya ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali itaweza kuimarisha udhibiti wa fedha na kuisaidia serikali kuimarisha uwajibikaji.

Kitabu hiki kinatoa majumuisho ya muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa taarifa za Fedha katika Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 na mawanda ya ukaguzi katika Serikali Kuu ambayo yanajumuisha Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Sekretarieti za Mikoa.

Pia, kuna majumuisho ya taarifa za ukaguzi katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kwa muhtasari, ambapo maelezo ya kina ya taarifa hizo yanapatikana katika taarifa za Halmashauri zilizotumwa kwa waheshimiwa wenyeviti wa Halmashauri na Maafisa masuuli husika.

Vilevile, ni muhtasari wa mkusanyiko wa ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine zilizofanyika kwa kipindi husika. Muhtasari huu unaainisha masuala yanayozorotesha ufanisi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kutekeleza na kufikia malengo waliyojiwekea.

Kitabu hiki pia kina muhtasari wa majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa miradi inayofadhiliwa na wahisani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miradi ipo katika makundi mawili ambayo ni miradi mikubwa minne yaani Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(TASAF), Mradi wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo(ASDP), Mradi wa Maendeleo wa Sekta ya Maji(WSDP) na Mfuko wa Sekta ya Afya (Health Basket Fund) na pia miradi mingine ambayo ni makubaliano kati ya Serikali na wahisani wengine.

Muhtasari mwingine ni kuhusu ripoti ya ukaguzi wa ufanisi (Value for money audit) ambapo inahusisha ripoti tano za kaguzi zilizofanyika Serikali Kuu (Idara ya Polisi na Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Kazi na Ajira na Wizara ya Fedha) ambazo ni Usimamizi wa Ukaguzi wa Magari na ukomo wa mwendo barabarani, Ukaguzi wa usimamizi wa Usalama Mahali pa kazi, Usimamizi wa Mikataba ya Miradi ya Ujenzi Katika Serikali za Mitaa, Usimamizi wa Manunuzi ya Vifaa vya TEHAMA Katika Sekta ya Umma na Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi Katika Ziwa Victoria.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa utaalamu, juhudi kubwa walioonyesha katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi vya kutosha, mishahara duni , upungufu wa watumishi na wakati mwingine kufanya kazi maeneo ya vijijini ambayo sio rahisi kufikika.

Pia, napenda kutambua kazi iliyofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, Kitengo cha Usimamizi wa Mali za Serikali na Msajili wa Hazina kwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za kiutendaji za Taasisi zilizoko chini yao kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 na kuonyesha mambo mengi ambayo kwa kiasi kikubwa yalijitokeza kwenye ripoti yangu ya mwaka uliopita.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti za ukaguzi jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu kwa siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

July, 2013

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA 2011/12

Toleo Maalum kwa Ajili ya Wananchi

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) ni taasisi pekee yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kama yalivyoidhinishwa na Bunge na pia kufanya ukaguzi wa thamani ya fedha (ufanisi) kwa mujibu wa Sheria. Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali katika kusimamia matumizi ya Rasilimali za Umma yameainishwa wazi kwenye ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa mara kwa mara), Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya 1982 (iliyorejewa 2000) na katika Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Ripoti za Ukaguzi za kila mwaka zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinalenga kutoa taarifa ili kuliwezesha Bunge kuisimamia vizuri Serikali katika kutekeleza jukumu lake juu ya usimamizi mzuri wa mapato na matumizi ya rasilimali za Umma.

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita (kuanzia mwaka 2007/2008), jamii imeanza kuona maboresho katika mchakato wa uwajibikaji nchini. Maboresho

haya yametokana na utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi pamoja na uwepo wa Kamati za Bunge za Kudumu ambazo zimesimamia na kuhimiza juu ya uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Ripoti za ukaguzi wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 ziliwasilishwa kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 28 Machi, 2013 na baadaye kuwasilishwa (tabled) bungeni na mawaziri husika tarehe 11 Aprili, 2013.

1.2 Rasilimali za Taifa (Umma)

Rasilimali za Taifa zinajumuisha fedha, maliasili ya nchi, watu, ardhi na mambo mengine yote yanayohitajika katika uendeshwaji wa Serikali kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Uwajibikaji katika rasilimali za Taifa ni dhana ya maadili na utawala bora.

1.3 Maana ya Uwajibikaji

Uwajibikaji kwa umma unatokana na majukumu ambayo wamepewa watu au taasisi walizokabidhiwa kusimamia rasilimali za taifa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mipango iliyopangwa kutekelezwa katika kipindi fulani cha utendaji.

Mihimili mikuu ya uwajibikaji ni pamoja na:

- Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambalo linawajibu wa kupitisha bajeti (kupanga na kugawa rasilimali za Taifa kwa taasisi mbalimbali) na kuisimamia Serikali katika makusanyo na matumizi ya rasilimali za Taifa zilizopitishwa na Bunge.

- Serikali (Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Bodi za Mashirika ya Umma), zinawajibu wa kukusanya na kutumia rasilimali za Taifa kama zilivyopitishwa na Bunge.

- Mahakama, inawajibu wa kusikiliza mashauri yote yanayofikishwa mahakamani na kutoa hukumu kulingana na sheria husika za nchi. Vilevile, mahakama inapokea na kusikiliza mashauri mbalimbali yanayohusiana na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Taifa kama vile Mahakama za Biashara, Ardhi n.k.

Serikali inatumia vyombo na makundi mbalimbali kwa ajili ya usimamizi wa matumizi ya Rasilimali za Taifa. Baadhi ya vyombo hivyo ni: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT), Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Sekretariati ya Maadili ya Viongozi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Wananchi wenyewe na vyombo vya habari. Vyombo hivi vinafanya kazi kwa karibu kabisa na Serikali pamoja na Bunge.

Kijitabu hiki ni muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 pamoja na taarifa za ukaguzi wa Ufanisi (Value for Money audit) kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2013.

SURA YA PILI

2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI

Ofisi yangu ina wajibu wa kukagua na kutoa maoni ya ukaguzi juu ya hesabu na kazi iliyofanyika kwenye Wizara, Idara, Taasisi, Shirika la Umma na Halmashauri. Maoni ya ukaguzi yanatolewa kama uthibitisho wa matokeo ya taarifa za ukaguzi wa fedha na ukaguzi wa ufanisi kwa kuangalia tija, ufanisi pamoja na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu zinazotakiwa katika kusimamia rasilimali za nchi

2.1 Hati za Ukaguzi

2.1.1 Maana ya Hati ya Ukaguzi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi yanayoelezea kama taarifa za fedha zilizokaguliwa zimetayarishwa kwa mujibu wa misingi inayokubalika katika uandaaji wa taarifa hizo. Hati ya ukaguzi inaelezea kama taarifa za fedha zilizowasilishwa zina maelezo ya kutosha.

2.1.2 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) na Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs), zifuatazo ni aina ya Hati za Ukaguzi zinazotolewa kama kipimo katika utayarishaji wa taarifa za fedha:

2.1.2.1 **Hati inayoridhisha (*Unqualified Opinion*)**

Hati hii inatolewa wakati ninaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika kimataifa.

2.1.2.2 Hati Inayoridhisha na yenye Suala la Msisitizo (*Unqualified Opinion with Emphasis of Matters*)

Hati hii inatolewa wakati ninaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi lakini kuna suala la msisitizo. Suala hilo halibadilishi hati ya ukaguzi kutoka hati inayoridhisha, bali linatoa msisitizo zaidi wa hali ilivyo ndani ya Wizara, Idara, Taasisi, Wakala, Shirika au Halmashauri iliyokaguliwa. Mfano wa masuala ya msisitizo ni kama vile, mambo ambayo yanaweza kuwa na athari baadae ambapo ufumbuzi wake unategemea maamuzi yaliyo nje ya Wizara, Idara, Taasisi, Wakala, Shirika au Halmashauri yenyewe na ambayo yanaweza kuleta athari katika taarifa za fedha hapo baadae. Vilevile, msisitizo unaweza kuwa wa masuala ambayo mkaguzi alipendekeza kwenye kaguzi zilizopita na bado hayajafanyiwa kazi na mkaguliwa.

2.1.2.3 Hati Yenye Shaka (*Qualified Opinion*)

Aina hii ya hati hutolewa pale ninapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za msingi katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka.

2.1.2.4 **Hati Yenye Shaka na Suala la Msisitizo (*Qualified Opinion with Emphasis of Matters*)**

Aina hii ya hati hutolewa pale ninapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za msingi katika usahihi wa hesabu.

Aya ya suala la msisitizo inaongezwa wakati kunahitajika uzingatiaji wa haraka kutoka kwa Watendaji Wakuu na watumiaji wa taarifa za fedha kuwatahadharisha kuhusu masuala yanayohitaji kushughulikiwa haraka na menejimenti.

2.1.2.5 **Hati Isiyoridhisha (*Adverse Opinion*)**

Hati isiyoridhisha inatolewa pale ninapoona kuwa, taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa ujumla wake hazikufuata viwango vinavyokubalika kiuhasibu vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, na zile zinazotolewa na Taasisi za Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa. Hati hii ni kinyume cha hati inayoridhisha. Kimsingi hati hii hueleza kwamba, taarifa zilizomo katika hesabu kwa kiasi kikubwa si sahihi wala za kuaminika kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha na matokeo ya kiutendaji ya Wizara, Idara, Taasisi, Wakala, Shirika au Halmashauri.

2.1.2.6 **Hati Mbaya (*Disclaimer Opinion*)**

Hati hii hutolewa pale ninaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Sababu zinazochangia kutolewa kwa hati hii ni pamoja na kukosa uhuru wa kufanya kazi ya ukaguzi ipasavyo, kuwa na wigo finyu wa kupata taarifa kwa ajili ya ukaguzi ama kwa kukusudia au kutokukusudia ambako kunazuia kazi ya mkaguzi kupata vielelezo vya kutosha. Hali hiyo inaathiri ukaguzi kiasi cha kumfanya mkaguzi kushindwa kutoa maoni ya hesabu hizo.

SURA YA TATU

3.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni, 2012.

3.1 Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za ukaguzi wa Serikali Kuu kwa miaka ya nyuma

Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zimekuwa na maendeleo mazuri katika utekelezaji wa masuala ya kaguzi za nyuma. Hata hivyo, katika mwaka huu wa ukaguzi, Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilikuwa hazijashughulikia masuala ya miaka ya nyuma yenye jumla ya Shilingi trilioni 2.007, Dola za Kimarekani milioni 2.12, Yeni za Kijapani bilioni 16.97 na Euro 850,000. Kati ya kiasi hicho, deni la Taifa na huduma za ujumla vinaongoza kwa kiasi kikubwa cha Shilingi bilioni 842.7 ikifuatiwa na Wizara ya Miundombinu yenye kiasi cha Shilingi bilioni 674.33 na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ikiwa ya tatu yenye kiasi cha Shilingi bilioni 85.14 na Euro 850,000.



3.2 Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa

Jumla ya Wizara 93 na Sekretarieti za Mikoa 21 zilikaguliwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 na matokeo yake ni kama ifuatavyo:

Mkaguliwa	Hati inayo-ridhisha	Hati inayori-dhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati yenye shaka	Hati isiyori-dhisha	Hati mbaya	Jumla
Wizara/Idara	40	47	6	0	0	93
Sekretarieti za Mikoa	7	14	0	0	0	21
Jumla	**47**	**61**	**6**	**0**	**0**	**114**

3.3 Mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka 2011/2012.

Katika ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka 2011/2012 mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na:

- Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa makampuni ya uchimbaji madini yalilipa mrahaba kwa kiwango cha asilimia 3% baada ya makato ikiwa ni kiwango cha sheria ya zamani ya madini badala ya asilimia 4% kabla ya makato kama inavyotakiwa na kipengele cha 87(1) I cha sheria ya madini ya mwaka 2010 ambayo imesababisha mapato ya mrahaba yasiokusanywa ya Shilingi bilioni 19.71.

- Madeni ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ya jumla ya Dola za Kimarekani milioni 41.47 yalikuwa hayajalipwa hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2011/12

- Malipo ya jumla ya bilioni 6.03 yalifanywa kwa kutumia vifungu vya bajeti visivyostahili na hivyo kuathiri majukumu yaliyokusudiwa kufanyika kwa fedha hizo.

- Deni la Taifa limeongezeka hadi kufikia Shilingi trilioni 16.98 mwaka 2011/2012 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 14.442 mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la Shilingi trilioni 2.065 (sawa na asilimia 17.6%).

- Idara ya Jeshi la Polisi haikuandaa mchanganuo wa manunuzi ya vifaa mbalimbali yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.34 hivyo haikuweza kuthibitika usahihi wa kiasi kilicholipwa kwa manunuzi haya kwenye mapato na matumizi ya fungu hili.

- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliuza viwanja 210 vyenye thamani ya Shilingi milioni 633.98 vilivyotengwa kwa waombaji mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam kutoka kipindi cha mwaka 2005 hadi 2011.

Ukaguzi wa kumbukumbu za uhasibu na nyaraka nyingine unaonyesha

kuwa hadi kufikia Juni, 2012 ni kiasi cha Shilingi milioni 209.64 tu kilikuwa kimekusanywa, na kuacha salio la Shilingi milioni 424.34 bila kukusanywa.

- Kampuni Saba za uwindaji yaani M/S Malagarasi Hunting Safaris, Mwanahuta & Company Ltd, Usangu Safaris Ltd, Rana Tours & Safaris Ltd, Coastal Wilderness (T) Ltd, Kilimanjaro Game Trails Ltd na Said Kawawa Hunting Company Ltd zina malimbikizo ya madeni ya dola za Kimarekani 973,493. Hadi natoa taarifa hii ya ukaguzi kampuni hizo bado zilikuwa zinaendelea kufanya kazi/shughuli za uwindaji huku zikiwa zinadaiwa deni hilo na Serikali.

- Misamaha ya kodi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa Shilingi trilioni

1.8 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 1.02 za mwaka 2010/2011 ikiwa ni sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 789.88 ambayo ni ongezeko la asilimia 78.



SURA YA NNE

4.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU - SERIKALI ZA MITAA

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri 134) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

4.1 Hoja za Halmashauri za miaka ya nyuma zisizojibiwa.

Serikali imejitahidi kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa za ukaguzi za miaka ya nyuma. Hata hivyo Halmashauri 131 kati ya 134 zilikuwa na hoja za miaka ya nyuma ambazo hazijatekelezwa. Kulikuwa na hoja za ukaguzi zilizohoji kiasi cha Shilingi bilioni 78.49 kwa mwaka 2011/2012 ambacho ni pungufu ya asilimia 25.46 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 105.263 zinazohusisha Halmashauri 130 zilizoripotiwa katika taarifa ya ukaguzi ya mwaka 2010/2011.

4.2 Mwelekeo wa jumla wa hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sehemu hii ya muhtasari inaonyesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2007/2008 hadi 2011/2012.

Umuhimu wa taarifa hii ni kuonyesha mwelekeo wa hali ya utendaji na uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Mchanganuo huo umeonyeshwa katika jedwali hapo chini kama ifuatavyo:-

HALI YA HATI ZA UKAGUZI KWENYE HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO 2007/2008 - 2011/2012

Miaka	Hati Zinazoridhisha		Hati zenye shaka		Hati Zisizoridhisha		Hati Mbaya		Idadi ya Halmashauri
	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	
2007/08	72	54	61	46	0	0	0	0	**133**
2008/09	77	58	55	41	1	1	0	0	**133**
2009/10	66	49	64	48	4	3	0	0	**134**
2010/11	72	54	56	42	5	4	0	0	**133**
2011/12	104	78	29	21	0	0	1	1	**134**

Kutokana na takrimu hizo hapo juu ni dhahiri kuwa Serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na utayarishaji wa hesabu za Halmashauri hata kuongeza hati za ukaguzi zinazoridhisha kutoka asimilia 54 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 78 mwaka 2011/2012 na kupunguza hati za ukaguzi zenye shaka kutoka asilimia 46 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 21 mwaka 2011/2012.

Maboresho haya ya Hati za ukaguzi zilizotolewa kwenye Mamlaka za Serikali za

Mitaa yametokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na:

Mikakati iliyowekwa na Serikali kwa ajili ya kushughulikia mapendekezo ya ripoti za CAG ikiwa ni pamoja na Waraka uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia TAMISEMI kusimamia kikamilifu uendeshaji wa shughuli za Serikali za Mitaa.

- Wananchi wamekuwa wakihitaji uwazi na uwajibikaji zaidi wa utendaji wa Halmashauri zao.

- Hatua madhubuti zinazochukuliwa na Taasisi za uchunguzi katika kutekeleza matakwa ya kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

- Kumekuwepo na uboreshaji wa taarifa za fedha zinazotolewa na Halmashauri kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma pamoja na uboreshaji wa Mfumo Funganishi wa IFMS – Epicor unaotumiwa na Serikali.

- Utendaji kazi mzuri wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

4.3 Mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Hesabu za Halmashauri kwa Mwaka 2011/2012.

Katika ukaguzi wa hesabu za Halmashauri kwa mwaka 2011/2012, mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na:

(i) Udhaifu katika Usimamizi wa Mapato ya Ndani

Usimamizi wa mapato kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa bado ni changamoto. Mapungufu mbalimbali yalibainika katika

eneo hili ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- Vitabu 2,990 vya stakabadhi (risiti) za mapato kutoka Halmashauri 36 havikutolewa kwa ajili ya ukaguzi.

- Halmashauri 56 zilikuwa na jumla ya Shilingi bilioni 4.47 ikiwa ni mapato yaliyokusanywa na mawakala ambayo yalikuwa bado hayajawasilishwa kwenye Halmashauri.

- Ulegevu katika udhibiti wa ndani wa Halmashauri 30 ulisababisha jumla ya Shilingi bilioni 8.01 kutoka kwa wadaiwa wa kodi mbalimbali za vyanzo vya ndani vya mapato kutokusanywa kama Kodi ya Huduma, ushuru wa mazao na ushuru wa Hoteli.

- Halmashauri 17 hazikukusanya kodi ya majengo kiasi cha Shilingi bilioni 4.35 ikiwa ni sawa na asilimia 38 ya makisio yaliofanywa.

(ii) Mapungufu katika usimamizi wa matumizi

- Halmashauri 22 kati ya 134 zilifanya malipo yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.51 ambayo hayakuwa na hati za malipo.

- Malipo yenye hati pungufu yalibainika katika Halmashauri 74 yenye jumla

ya Shilingi bilioni 3.37

- Jumla ya Shilingi milioni 650.36 katika Halmashauri 20 zililipwa kwa Taasisi mbali mbali na katika ngazi za Vijiji lakini fedha hizo hazikuthibitika kupokelewa kutokana na kukosekana kwa stakabadhi (risiti) za mapokezi ya fedha hizo.

(iii) Mapungufu katika menejimenti ya rasilimali watu (watumishi) na udhibiti wa mishahara

- Katika sampuli ya Halmashauri 25 ilibainika kuwepo uhaba wa watumishi 14,663 ikilinganishwa na idadi inayotakiwa ya watumishi 73,087 kwa mujibu wa ikama ilivyoidhinishwa. Upungufu wa idadi ya watumishi una athari katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri. Athari hizo ni kama vile kutotoa huduma katika kiwango kinachohitajika.

- Jumla ya Shilingi milioni 693.13 zililipwa kama mishahara kwa wastaafu, watoro, watumishi waliofariki, watumishi walioacha kazi au walioachishwa kazi kupitia akaunti zao za benki. Malipo hayo yamehusisha jumla ya Halmashauri 43.



- Ukaguzi wa mwaka huu umebaini kuwa mishahara ya baadhi ya watumishi wa Halmashauri inakatwa hadi kufikia kiasi kinachozidi theluthi mbili (2/3) kwa sababu ya ukopaji uliokithiri kutoka kwenye taasisi za fedha na asasi nyinginezo. Katika Halmashauri nyingine, kuna watumishi waliokuwa hawalipwi chochote kabisa kama mshahara kutokana na makato hayo. Ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri 87 umeonyesha kuwa zaidi ya watumishi 17,710 walikuwa wakipokea pungufu ya theluthi moja ya mishahara yao kinyume na miongozo ya utumishi.

(iv) Kuwepo kwa udhaifu katika uzingatiaji wa taratibu na Sheria za Manunuzi

- Manunuzi yenye thamani ya Shilingi milioni 443.11 katika Halmashauri 25 yalifanyika kutoka kwa wauzaji mbalimbali wa bidhaa na huduma bila ushindani wa bei.

- Ununuzi wa bidhaa na huduma za thamani ya Shilingi milioni 541.01 ulifanyika bila kibali cha Bodi za Zabuni katika Halmashauri 24.

(v) Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)

Jumla ya Shilingi bilioni 2.56 zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo hazikutumika katika sampuli ya Halmashauri 69

zilizokaguliwa.

(vi) Mapungufu katika utekelezaji wa Bajeti

- Bunge lilipitisha bajeti kwa baadhi ya vifungu vya fedha za maendeleo vyenye jumla ya Shilingi bilioni 595.06 katika Halmashauri 113. Hata hivyo, ni Shilingi bilioni 345.57 tu ndizo zilizopokelewa na Halmashauri husika, na kufanya kuwepo upungufu wa Shilingi bilioni 249.5 sawa na asilimia 42. Hadi mwisho wa mwaka kulikuwa na salio la fedha za miradi ya maendeleo ya Halmashauri 132 kiasi cha Shilingi bilioni 188.41 ambayo ni sawa na asilimia 55 ya kiasi cha fedha zilizokuwepo katika mwaka husika.

4.4 Matokeo ya kaguzi maalum

Matokeo ya kaguzi maalum katika Halmashauri 14 zilizofanywa na ofisi yangu ni kama ilivyoainishwa hapa chini:

- Hati za malipo za Shilingi bilioni 4.996 na viambatisho vyenye jumla ya Shilingi bilioni 1.08 havikuwasilishwa wakati wa Ukaguzi.

- Malipo ya Shilingi milioni 82.37 ya mishahara yalifanyika kwa watumishi ambao hawako katika utumishi wa Serikali na majina yao hayajafutwa katika orodha ya mishahara.

- Kutokuwa na uaminifu katika sehemu za kazi kumepelekea baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kufanya ubadhirifu wa Shilingi milioni 23.22 na watumishi wengine kuwa na kesi ya kugushi ya Shilingi milioni 12.74

- Mapato zaidi ya Shilingi bilioni 3.89 katika Manispaa ya Arusha yamepotea kutokana na Halmashauri hiyo kutoza kiwango kidogo cha kodi kwenye vyumba/vibanda vya biashara ambavyo vinamilikiwa na Halmashauri ambayo ni tofauti kubwa ukilinganisha na bei ya soko.

- Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ilitumia salio la ruzuku ya mishahara

Shilingi milioni 452.02 katika matumizi mengine kinyume na utaratibu wa kuzirudisha Hazina.

- Kiasi cha ziada cha Shilingi milioni 97.12 kililipwa kwa mkandarasi wa ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi, ujenzi wa jengo la utawala la hospitali na ujenzi wa jengo la ofisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kutokana na vipimo vya ziada vilivyoonekana kwenye makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) baada ya kupima upya majengo.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni, 2012.

5.1 **Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za ukaguzi wa mashirika ya umma kwa miaka ya nyuma**

Katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa za ukaguzi za miaka ya nyuma kuanzia mwaka 2007/2008 hadi mwaka 2010/11 Serikali haikuwa imeyafanyia kazi mapendekezo yafuatayo:

- Kuchelewa kuteua Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za serikali.
- Wabunge kutoteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma ili kuondoa migongano ya kimaslahi.

- Kutokuwepo na mikataba ya utendaji kati ya Serikali na Wakurugenzi Watendaji wa Mashirika ya Umma.

- Kutorejeshwa kwa mkopo wa PSPF wa Shilingi bilioni 58 uliokopwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

- Ucheleweshwaji wa fedha za bajeti ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Hazina.

5.2 Ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2011/2012

5.2.1 Hali ya Ukaguzi na Ripoti Zilizokaguliwa

Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2013 nilikamilisha kaguzi 126 kati ya 176 zinazotakiwa kukaguliwa ikiwa ni sawa na asilimia 71.6. Kaguzi za Taasisi 50 ziko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Katika kaguzi zilizokamilika, ripoti 95 zilikuwa zimeshasainiwa wakati ripoti 31 zilikuwa zinasubiri hesabu kuridhiwa na kusainiwa na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika.

5.3 Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma

5.3.1 Matokeo ya kaguzi zilizokamilika yalikuwa ni kama ifuatavyo:

Mwaka wa Ukaguzi	Hati inay-or-id-hisha	Hati inayori-dhisha yenye msisitizo	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka na msisiti-zo	Hati kush-indwa kutolewa (Hati mbaya)	Hati isiyo-ri-dhi-sha	Jumla ya Mashiri-ka
2009/2010	**92**	**12**	**10**	**7**	**1**	**0**	**122**
Asilimia (%)	75.4	9.8	8.2	5.8	0.8	0	100

2010/2011	**84**	**12**	**7**	**4**	**0**	**0**	**107**
Asilimia (%)	78.5	11.3	6.5	3.7	0	0	100
2011/2012	**62**	**23**	**2**	**7**	**1**	**0**	**95**
Asilimia (%)	65.3	24.2	2.1	7.4	1	0	100

5.4 Mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Hesabu za Mwaka 2011/2012.

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka 2011/2012, mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa matukio ya uwindaji haramu katika Hifadhi za Taifa (TANAPA)

Ripoti za robo mwaka za idara ya ulinzi za Mamlaka ya Hifadhi za Taifa TANAPA zilionyesha kuwa vitendo vya uwindaji haramu hususani tembo vimeongezeka sana ambapo jumla ya Tembo 110 waliuwawa. Hii ina athari kubwa katika juhudi za serikali za kuendeleza utalii na kuongeza pato la Taifa.

(ii) **Bodi ya Huduma ya Maktaba Tanzania (TLSB) kushindwa kutoa Bandarini Kontena mbili za vitabu tangu mwaka 2009 vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la kufadhili Watoto**

Kulingana na maelezo ya Menejimenti ya TLSB, gharama za awali za kutolea kontena hizo bandarini zilikuwa zimefikia kiasi cha Shilingi milioni 147. Deni halisi la kugomboa vitabu hivyo kwa sasa halikupatikana kwa ajili ya uhakiki.

(iii) **Malipo yasiyo na faida ya Shilingi bilioni 2.24 yaliyolipwa kwa Mkandarasi baada ya kusitishwa kwa mkataba na Mamlaka ya Bandari**

Mamlaka ya Bandari Tanzania ililipa Shilingi bilioni 2.24 ikiwa ni faini kwa mkandarasi (Oceana Advanced Industries Ltd) kutokana na kushindwa kumkabidhi Mkandarasi eneo husika la kazi kutokana na kutofanyika utafiti wa kina kabla ya kutoa zabuni husika. Katika mkataba huu fedha zilizolipwa Shilingi bilioni 2.24 hazikuwa na manufaa yoyote kwa Shirika wala Serikali (nugatory expenditure).

(iv) **Malipo tata ya leseni ya biashara yaliyolipwa na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kwa niaba ya Kampuni ya Star Media (SMT) Shilingi milioni 618.3**

Ukaguzi ulibaini kwamba mwaka 2010 TBC ililipa Shilingi milioni 618.3 kwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa niaba ya Kampuni ya SMT kwa ajili ya leseni ya biashara. Pia Ukaguzi umebaini kwamba kampuni hiyo ina mkataba wa utendaji uliosainiwa na Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) ambapo SMT imepewa msamaha wa kulipa leseni ya biashara kwa kipindi cha miaka kumi. Kiasi kilicholipwa na TBC kwa TCRA kwa niaba ya kampuni ya SMT kingeweza kuwa ni sehemu ya hisa za shirika (TBC) kwa SMT. Hivyo inashauriwa TBC irejeshe fedha hizo kutoka kwa TCRA na zitumike katika kununua hisa za kampuni ya SMT.

(v) **Hali isiyoridhisha ya mwenendo wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF)**

Katika ukaguzi wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu nilibaini kwamba ukadiriaji thamani uliofanywa na Kampuni ya Uthaminishaji ya Genesis Acturial Solution Limited na kutoa ripoti yake tarehe 30 Juni, 2010 uliashiria kwamba uwezo wa kifedha wa PSPF uliendelea kushuka. Ukadiriaji thamani huo ulibaini malimbikizo ya mafao ya Shilingi trilioni 6.487 hivyo Mfuko uko kwenye hatari ya kutoweza kujiendesha kama juhudi za makusudi hazitachukuliwa na Serikali za kurekebisha hali hiyo.

Pamoja na Mfuko kuwa katika hali mbaya kifedha, nilibaini kuwa Mfuko ulitoa mikopo kwa Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine ambayo imedhaminiwa na Serikali yenye jumla ya Shilingi bilioni 67.2 bila kujumuisha riba. Madeni yasiyolipika bila kujumuisha riba yameonyeshwa katika jedwali hapa chini;

Mikopo ambayo haijalipwa

Na.	Jina la Mkopaji	Sekta	Salio (Sh.)
1	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa elimu ya juu	Taasisi ya Serikali	54,644,657,534
2	TAKUKURU	Taasisi ya Serikali	6,678,150,000
3	Tan Power Resources	Taasisi isiyo ya Kiserikali	5,421,551,370
4	Kiwanda cha Madawa Tanzania	Taasisi isiyo ya Kiserikali	435,057,632
Jumla Kuu			**67,179,416,536**

(vi) **Wizara ya Maliasili na Utalii kuingilia Utendaji wa Bodi ya Utalii**

Katika ukaguzi uliofanyika nilibaini kuwepo kwa shughuli zinazoashiria Wizara ya Maliasili na Utalii kuingilia utendaji wa shughuli za Bodi ya Utalii. Kwa mfano Wizara ilihamisha jumla ya Shilingi milioni 771.2 kwenda Bodi ya Utalii kwa shughuli ambazo siyo za Bodi ya Utalii. Fedha hizi zilichukuliwa kwa maelekezo na maagizo kutoka Wizarani. Jambo la kushangaza zaidi ni

pale ambapo jumla ya Shilingi milioni 416.1 zilichukuliwa kutoka Bodi ya Utalii na wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Shilingi milioni 355.1 zililipwa moja kwa moja kwa idara nyingine au watoa huduma wengine kwa maelekezo ya Wizara. Muingiliano kama huu katika shughuli za kiutendaji katika Mashirika ya Umma unakwamisha uwajibikaji katika shughuli za taasisi hizo.

(vii) **Matumizi Mabaya ya Madaraka**

Kampuni ya McDonald Live Line Technology Limited ilipewa zabuni na TANESCO wakati ilikuwa na makubaliano ya ubia na Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO wa wakati huo. Kampuni hiyo ilipewa mikataba ya kukarabati na kutengeneza njia za umeme hai, mikataba iliyosainiwa mwaka 2008 hadi 2011. Ilikuwa kinyume na Kanuni za maadili ya TANESCO na Kanuni za maadili za viongozi za mwaka 1995 kwa Mkurugenzi wa TANESCO kuipa Mikataba ya kazi kampuni ya McDonald Live Line Technology Limited ambayo yeye ni mbia.

Uthibitisho kutoka BRELA ulionyesha kwamba Kampuni ya McDonald Live Line Technology Ltd haikuwasilisha mrejesho wowote wa hesabu au utendaji kwa miaka ya 2005 hadi 2011. Kiasi cha Shilingi bilioni 1.12 kililipwa kwa McDonald kwa mikataba iliyosainiwa mwaka 2008 hadi 2011

na TANESCO. Malipo hayo ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya kiasi cha Shilingi milioni 168.9 ambacho hakikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

(viii) **Uuzwaji wa Hisa za kampuni ya Usafiri Dar es Salaam (UDA)**

Ukaguzi Maalum wa uuzwaji wa hisa za UDA kwa Kampuni ya Mwekezaji ulibaini kuwa Bodi ya Wakurugenzi wa UDA haikuzingatia taratibu za Sheria ya Manunuzi katika kuuza hisa za UDA kwa Kampuni ya Mwekezaji. Hisa za UDA zilifanyiwa makadirio ya thamani ya Shilingi 744.79 mnamo mwezi Octoba, 2009 kwa hisa moja. Hata hivyo, hisa hizo ziliuzwa kwa Kampuni ya Mwekezaji kwa Shilingi 145 kwa hisa moja, bila kuzingatia makadirio ya thamani yaliyokwishafanyika. Kiasi cha fedha kilichotakiwa kulipwa kwa bei hiyo ya punguzo ilikuwa ni Shilingi bilioni 1.14 lakini ni kiasi cha Shilingi milioni 285 tu ndicho kilicholipwa na salio lililobaki bado halijalipwa na Mwekezaji huyo. Kampuni Hodhi ya Mashirika ya Umma (CHC) ndiyo ilikuwa na Mamlaka ya kuidhinisha uuzaji wa hisa za UDA na siyo Bodi ya Wakurugenzi wa UDA kama ilivyofanyika. Bodi ya Wakurugenzi ya UDA ilipuuza ushauri wa kitaalamu uliotolewa na CHC na kuendelea na mchakato wa kuuza hisa za shirika.

Aidha, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa UDA alipokea kiasi cha Shilingi milioni 320 kwa kile kilichoelezewa ni malipo ya kutoa huduma ya ushauri (Consultancy Service) kwa Kampuni ya Mwekezaji ambayo hali hiyo inaleta moja kwa moja mgongano wa kimaslahi mkubwa kwa Mwenyekiti huyo kwa kuwa yeye kama Mwenyekiti wa Bodi hangeweza

kumpa ushauri Mwekezaji anaenunua hisa za Shirika analoongoza.

(ix) **Usimamizi Usioridhisha Katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania**

Ukaguzi uliofanyika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania uligundua udhaifu mkubwa ambao unahitaji hatua za haraka kuchukuliwa.

Katika kupitia taarifa za mkaguzi wa ndani, nilibaini kwamba ripoti ya uchunguzi ya mkaguzi wa ndani ilionyesha ubadhilifu wa fedha za umma jumla ya Shilingi milioni 700.2.

SURA YA SITA

6.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioisha tarehe 30 Juni, 2012.

6.1 Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa miaka ya nyuma

6.1.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

Katika ukaguzi wa mwaka huu, Halmashauri 64 zilikuwa na masuala ya miaka ya nyuma yanayohusu Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo yenye thamani ya Shilingi bilioni 9.087 ambayo hayajatekelezwa.

6.1.2 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

Katika ukaguzi wa mwaka huu, Halmashauri 14 zilikuwa na masuala ya miaka ya nyuma yanayohusu Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji yenye thamani ya Shilingi milioni 220.078 ambayo hayajatekelezwa.

6.1.3 **Mfuko wa Maendeleo ya Afya**

Katika ukaguzi wa mwaka huu, Halmashauri 79 zilikuwa na masuala ya miaka ya nyuma yanayohusu Mfuko wa Maendeleo ya Afya yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.982 ambayo hayajatekelezwa.

6.2 Mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa

Jedwali hapa chini linaonyesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka 2011/2012.

Mkaguliwa	Hati zinazoridhisha bila maswala ya msisitizo	Hati zinazoridhisha na maswala ya msisitizo	Hati zenye Shaka	Hati zisizoridhisha	Hati mbaya	Jumla
TASAF	28	75	24	0	0	127
Asilimia (%)	22.05	59.05	18.9	0	0	100
ASDP	17	82	33	0	0	132
Asilimia (%)	12.88	62.12	25	0	0	100
WSDP	10	95	25	1	0	131
Asilimia (%)	7.63	72.52	19.08	0.77	0	100
HBF	6	94	32	0	0	132
Asilimia (%)	4.55	71.21	24.24	0	0	100
Jumla ndogo	**61**	**346**	**114**	**1**	**0**	**522**
Asilimia (%)	**11.69**	**66.28**	**21.84**	**0.19**	**0**	**100**
Miradi mingine	68	22	3	0	0	93
Asilimia (%)	73.12	23.65	3.23	0	0	100
Jumla Kuu	**129**	**368**	**117**	**1**	**0**	**615**

6.3 Mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Hesabu za Mwaka 2011/2012.

6.3.1 Mapungufu katika taratibu na mikataba ya manunuzi

(i) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

- **Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi za Zabuni**

  Ilibainika kuwa Halmashauri saba (7) zilifanya manunuzi ya kiasi cha Shilingi milioni 270.1 bila idhini ya Bodi za Zabuni. Hii inatokana na usimamizi mbovu wa mikataba kinyume na kanuni Na. 40 na 41 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.

- **Manunuzi yaliyofanywa bila kushindanisha Wazabuni Shilingi milioni 252.94**

  Halmashauri nane (8) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi milioni 252.94 bila kushindanisha wazabuni. Hii ni kinyume naKanuni ya 28 ya Kanuni za manunuzi ya umma, 2005.

(ii) Mfuko wa Maendeleo ya Afya (HBF):

- **Mali na vifaa vyenye thamani ya Shilingi milioni 180.703 havijapokelewa**

  Mali na vifaa vya thamani ya Shilingi milioni 180.703 vilivyonunuliwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Afya havijapokelewa kinyume na Kanuni 122 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2005 inayosisitiza uwepo wa taarifa ya kupokea vifaa kwanza na baadaye malipo kuidhinishwa.

- **Manunuzi ya Dawa na vifaa vya tiba kutoka kwa wazabuni binafsi bila kibali cha Bohari Kuu ya Dawa Shilingi milioni 412.22**

  Kiasi cha Shilingi milioni 412.22 kililipwa na Halmashauri kumi(10) ikiwa ni manunuzi ya dawa na vifaa vya tiba kwa wazabuni binafsi bila kibali cha Bohari Kuu ya Dawa kinyume na kifungu 3.5 (h) sura ya tatu ya Mwongozo wa Mkakati Maalumu wa Afya kwa Halmashauri wa mwaka, 2007.

(iii) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF):

- Ilibainika kuwa kuna manunuzi ya mali na vifaa vyenye thamani ya Shilingi milioni 50.275 ambavyo havikupokelewa

- Mapitio ya mfumo wa manunuzi na mapokezi ya mali na vifaa ulibaini kuwepo kwa udhaifu wa kutokuwepo ushindani wa bei, manunuzi yalifanyika bila kufuata mpango, na vifaa vilivyonunuliwa havikupokelewa na kuingizwa kwenye daftari.

- Ilibainika kuwa katika miradi sita ya manispaa ya Kigoma iliyotembelewa yenye thamani ya Shilingi milioni 76.513 mchanganuo wa gharama za kazi haukuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

- Katika Mradi wa Mabasi ya Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) mradi ulitoa kazi ya ujenzi na ulinzi ya thamani ya Shilingi milioni 111.03 bila idhini ya Bodi ya Zabuni na hapakuwepo mikataba.

(iv) Mradi wa Sayansi na Teknolojia Elimu ya Juu (STHEP)

Menejimenti ya COSTECH ilinunua jenereta mpya lenye uwezo wa 200KV kutoka INCAR TANZANIA LTD kwa gharama ya kiasi cha dola za kimarekani 58,797.88. Mzabuni alilipwa kabla ya kufanya ukaguzi na matokeo yake jenereta iliyoletwa haikuwa katika viwango vilivyoainishwa kiufundi.

6.3.2 Mapungufu na udhaifu katika usimamizi wa fedha

(i) Mapungufu katika Sekta ya kilimo

- **Malipo yasiyokubalika Shilingi bilioni 1.026**

  Halmashauri thelathini na saba (37) zilifanya malipo ya kiasi cha Shilingi bilioni 1.026 bila kuwa na nyaraka halisi ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

- **Malipo yenye nyaraka pungufu Shilingi milioni 394.055**

  Kulikuwa na malipo ya Shilingi milioni 394.055 yenye nyaraka pungufu kutoka kwenye Halmashauri 26 tulizozikagua.

- **Hati za malipo zisizokaguliwa Shilingi milioni 320.062**

  Hati za malipo (vocha) za thamani ya Shilingi milioni 320.062 zilizoandikwa kwenye daftari la fedha hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi katika Halmashauri tisa (9). Hii ni kinyume na Kifungu 45(5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Halmashauri ya Mbarali ilikuwa na asilimia 74, ikifuatiwa na Bunda yenye asilimia 8.73 na ya tatu ni Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo yenye asilimia 4. Usahihi na uhalali wa malipo yaliyofanyika haukuweza kuthibitishwa.

(ii) Mapungufu katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

- **Malipo yasiyokubalika yenye thamani ya Shilingi milioni 353.037**

  Malipo yasiyokubalika ya jumla ya Shilingi 353.037 milioni yalifanyika katika Halmashauri kumi (10) kwa manufaa yasiyokuwa ya mradi kinyume na makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Wadau wa Maendeleo ambapo sehemu namba 9.2.2 ya makubaliano hayo kinazuia ulipaji kodi kutoka kwenye fedha za mradi.

- **Malipo yenye nyaraka pungufu yenye thamani ya Shilingi milioni 421. 638**

  Kulikuwa na malipo yenye nyaraka pungufu ya jumla ya kiasi cha Shilingi 421.638 milioni yaliyofanywa kinyume na kifungu namba 45 (5) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 pamoja na Agizo Namba 8(2)(c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (2009).

(iii) Mapungufu katika Mfuko wa Maendeleo ya Afya

- **Kukosekana kwa hati za malipo zenye thamani ya Shilingi 296.087 milioni**

  Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, matumizi ya Shilingi 296.087 milioni yalifanywa bila kuwepo hati za malipo, hivyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa. Halmashauri tatu (3) ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mbarali na Halmashauri ya Jiji la Mbeya zilifanya malipo bila kutumia hati za malipo na kukiuka kifungu cha 34(i) cha Mwongozo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009.

- **Malipo yenye hati pungufu yenye thamani ya Shilingi milioni 271.065**

Ukaguzi wa hati za malipo na viambatisho vyake ulibaini kuwa malipo ya Shilingi milioni 271.065 yana hati pungufu na yamekosa viambatisho vinavyohusika. Hii ni kinyume na Mwongozo wa uhasibu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Aya ya 2.4.1 ambao unaagiza malipo yote yanayolipwa na Halmashauri yawe na viambatisho muhimu.

(iv) Mapungufu katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF)

- Matumizi yenye thamani ya Shilingi milioni 14.263 yalilipwa kwenye vifungu visivyo husika

- **Malipo yenye thamani ya Shilingi milioni 224.355 yalikuwa na hati pungufu na mengine hayakuwa na hati kabisa**

  Ukaguzi wa hati za malipo ulibaini kuwepo kwa malipo yenye thamani ya Shilingi milioni 153.344 ambayo hayakuwa na viambatisho vinavyohusika. Hii ni kinyume na Agizo Na. 10(2)(d) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Aidha, kulikuwa na malipo yenye thamani ya Shilingi milioni 71.01 ambayo hati zake za malipo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kinyume na Agizo Na.104 (2) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Katika mazingira haya, uhakika na uhalali wa hayo matumizi haukuweza kuthibitika.

(v) Mapungufu katika Mfuko wa Kimataifa wa kupambana na UKIMWI, MALARIA, KIFUA KIKUU na UKOMA.

- **Matumizi batili ya kiasi cha dola za Kimarekani 16,976.80**

Ukaguzi ulibaini malipo ya kiasi cha dola za kimarekani 16,976.80 kwa ajili ya matumizi ya posho, vifaa vya usafi na gharama za semina. Matumizi haya hayakustahili kulipwa na fedha za mradi kulingana na aya 9.1 na 9.5 ya mpango wa utekelezaji mradi.

- **Malipo yenye nyaraka pungufu yenye thamani ya dola za Kimarekani 154,071.29**

Ukaguzi wa hati za malipo na viambatisho vyake umebaini malipo yenye thamani ya dola za Kimarekani 154,071.29 ambayo yana hati pungufu na yamekosa viambatisho vinavyohusika. Hii ni kinyume na programu na mpango wa utekelezaji wa mradi. Katika mazingira haya, uhakika na uhalali wa matumizi hayo haukuweza kuthibitika.

(vi) Mapungufu katika Ukarabati wa Miundombinu ya Afya Wilayani

- **Malipo yenye nyaraka pungufu ya Shilingi milioni 43.808**

Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha Shilingi milioni 43.808 kililipwa kwa Baraza la Ujenzi la Taifa kupitia benki ya NMB tawi la Dodoma ikiwa ni ada ya ushauri. Hata hivyo malipo haya yalifanyika bila kuwa kwenye bajeti, hayakuwa na hati ya madai, malipo yalilipwa kufuta madeni ya miaka ya nyuma ambayo wadeni hawakuonyeshwa kwenye orodha

ya wadeni, hapakuwa na stakabadhi ya kukiri mapokezi ya fedha hizo na malipo hayakuwa na mkataba.



(vii) Mapungufu katika Mradi wa kufundisha Mafunzo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza katika Shule za Sekondari za Serikali kwa kutumia TEHAMA.

- **Matumizi batili kiasi cha Shilingi milioni 30.8**

  Malipo ya kiasi cha Shilingi milioni 30.8 yalifanyika kama gharama ya uzinduzi wa mradi wa kufundisha na kujifunza sayansi, hisabati na kiingereza katika shule za sekondari kwa njia ya TEHAMA. Uzinduzi wa mradi huu ulifanyika kuanzia tarehe 26/09/2011 hadi 27/09/2011. Hata hivyo, kulingana na kifungu 4 na 5 cha makubaliano katika mkataba, gharama za uzinduzi hazikutakiwa kulipwa na fedha ya mradi.

(viii) Mapungufu katika Mradi wa Mtandao wa Maabara za Umma kanda ya Afrika Mashariki

- **Matumizi batili ya kiasi cha Shilingi milioni 72**

  Kiasi cha Shilingi milioni 72 kililipwa na mradi ikiwa ni posho za vikao, posho za "honoraria", posho za warsha na posho za mkutano wa kamati kuu ya mradi. Malipo haya yalikuwa kinyume na maelekezo ya Benki ya Dunia ya tarehe 5/7/2011 yanayozuia malipo ya posho za aina hii.

(ix) Mapungufu katika Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani na Bahari

- **Matumizi batili ya Shilingi milioni 124.78**

Kiasi cha Shilingi milioni 444.75 kililipwa kwa wazabuni wa samani, Ujenzi na vifaa vya ofisi kwa ajili ya mradi wa MACEMP. Kati ya malipo haya kiasi cha Shilingi milioni 124.78 kilihusu kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo haikutakiwa kulipwa kulingana na kifungu 5.08 cha mkataba wa mkopo, hivyo malipo haya ni batili.

(x) Mapungufu katika mradi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania

- **Malipo yenye nyaraka pungufu Shilingi milioni 33.81**

Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania, ililipa kiasi cha Shilingi milioni 33.81 kutekeleza kazi za mradi. Ukaguzi ulibaini kwamba malipo haya yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na kanuni 95(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa mwaka, 2004).

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA UFANISI NA UKAGUZI MAALUM

Ripoti ya Ukaguzi kwa mwaka 2011/12

SURA YA SABA

7.0 UTANGULIZI

Taarifa ya awali

Kaguzi za ufanisi ni muhimu kwa sababu zinalenga kuboresha uwajibikaji na utendaji wa taasisi za serikali ili wananchi wapate huduma zinazolingana na thamani ya fedha. Kuna vigezo ambavyo hutumika katika kuchagua maeneo ya kufanya kaguzi za ufanisi na kaguzi maalumu. Miongoni mwa vigezo hivyo ni pamoja na kilio cha umma na umuhimu wa eneo husika kwa sababu za kijamii na kiuchumi.

Ripoti hii ya ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi maalumu inazungumzia muhtasari wa kaguzi tano ambazo ni ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Magari na ukomo wa mwendo kasi, ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Afya na Usalama mahali pa kazi hasa ikilenga katika usajili na ukaguzi wa mahali pa kazi Tanzania, ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa mikataba ya miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa, ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma na ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Victoria.

7.1 USIMAMIZI WA UKAGUZI WA MAGARI NA UKOMO WA MWENDO BARABARANI

7.1.1 Uchunguzi Uliofanyika

Ukaguzi ulichunguza kama ukaguzi wa magari na ukomo wa mwendo barabarani ulilenga vihatarishi na ulisimamiwa ipasavyo kitija na kiufanisi na Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani. Ukaguzi uliangalia mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa ukomo wa mwendo barabarani.

Jeshi la Polisi Kitengo cha usalama barabarani Makao Makuu na Wizara ya Ujenzi kupitia Kurugenzi ya Usalama Barabarani na Mazingira walikuwa ndio wakaguliwa wakuu. Ukaguzi pia uliwahusisha wahusika wengine muhimu katika Usimamizi wa Usalama Barabarani na Mazingira ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya kudhibiti Usafiri wa Majini na Nchi Kavu 'SUMATRA' na Wakala wa Barabara Tanzania 'TANROADS'.

Ukaguzi ulilenga kipindi cha miaka minne kuanzia Januari, 2007 - Desemba, 2010. Takwimu zilikusanywa kutoka mikoa tisa (9) kati ya 21 ya Tanzania Bara. Barabara sita (6), za Mkoa na Wilaya zilihusishwa wakati wa ukaguzi huu ikiwa ni pamoja na abiria na magari ya mizigo.

7.1.2 **Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi**

(i) Ukaguzi wa magari haulengi kutosheleza vihatarishi vikuu vya ajali

Ukaguzi ulibainisha kuwa ukaguzi wa magari haukuweka kipaumbele kushughulikia mambo makubwa ambayo yanachangia ajali za barabarani. Kipaumbele kiliwekwa katika mambo ambayo hayapelekei kupunguza ajali za barabarani. Sababu za kibinadamu zilichangia kiasi cha asilimia 74 ya ajali zote zilizotokea barabarani nchini Tanzania katika mwaka 2010, lakini sababu hii haipewi kipaumbele kinachostaili.

(ii) Madereva kurudia makosa

Malengo ya kuweka adhabu hayakuweza kufikiwa kwani madereva wengi waliendelea kurudia kutenda makosa yale yale waliyokwisha tenda na kupewa adhabu. Kati ya madereva 445 walioitikia katika dodoso letu madereva 297 walikiri kurudia makosa yaleyale kwa zaidi ya mara tatu katika mwaka mmoja.

(iii) Rasilimali za Polisi hazigawanywi kulingana na vihatarishi katika ajali za barabarani

Ilibainika kwamba Jeshi la Polisi halizingatii mgawanyo wa rasilimali zake kulingana na kiwango cha vihatarishi katika eneo husika. Mgawanyo wa askari wa usalama

barabarani na vifaa vya ukaguzi kama vile bunduki, vipimia kasi ya mwendo na vipima ulevi wa madereva haukufanyika kwa kuzingatia vihatarishi katika ajali za barabarani.

(iv) Udhaifu katika Ufuatiliaji na ufanyaji tathmini

Ukaguzi unaofanywa na polisi wa barabarani haujafanyiwa tathmini kuangalia kama matakwa ya ukaguzi na malengo yanafikiwa. Wizara ya Ujenzi haijaweza kufanya mapitio ya muda katika ukomo wa mwendo wa barabarani nchini kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita.

7.1.3 Mapendekezo ya ukaguzi

(i) Jeshi la Polisi Tanzania linatakiwa kuhakikisha kuwa linapanga ipasavyo ukaguzi wake kwa kulenga barabara na maeneo ambayo ajali za barabarani zinatokea mara kwa mara zaidi ikilinganishwa na sehemu nyingine.

(ii) Ukaguzi wa usalama barabarani uzingatie vipaumbele kulingana na hatari zilizopo kama vile mwendo kasi na ulevi.

(iii) Taarifa ya ajali za barabarani zikusanywe kwa usahihi na kikamilifu ili ziweze kutumika katika uchambuzi wa uhandisi na kusaidia katika mashtaka ya kisheria.

(iv) Maeneo yote yenye hatari kubwa ya ajali za barabarani yapewe kipaumbele cha juu katika mgao wa rasilimali za ukaguzi wa usalama barabarani (rasilimali watu, fedha, zana za ukaguzi na magari).

(v) Jeshi la Polisi Tanzania linapaswa kuhakikisha kwamba matumizi ya adhabu kwa wavunja sheria wa barabarani yanatumika ipasavyo kwa mujibu wa sheria na kanuni kama zilivyoainishwa. Pia jeshi la Polisi liwe na njia ya kutathmini ufanisi wa adhabu zinazotolewa. Vile vile Jeshi la Polisi liwe na mfumo wa kuweka historia ya madereva na adhabu wanazotozwa ili wawajue madereva wakorofi zaidi yaw engine.

(vi) Wizara ya Ujenzi ihakikishe kwamba alama za mipaka ya mwendo wa magari katika barabara mbalimbali zinawekwa vizuri, kulingana na aina ya barabara na hali na mazingira yake.

7.2 UKAGUZI WA USIMAMIZI WA USALAMA MAHALI PA KAZI

7.2.1 **Uchunguzi Uliofanyika**

Ukaguzi ulichunguza kama Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) inasimamia ipasavyo ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi. Ukaguzi ulijikita katika mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa usalama mahali pa kazi na mgawanyo wa rasilimali. Takwimu zilikusanywa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai, 2009 mpaka Juni, 2012.

7.2.2 **Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi:**

(i) Ukaguzi ulibaini kuwa OSHA iliweza kusajili asilimia 24 tu ya maeneo ya kazi yanayokadiriwa kuwepo. Pia ukaguzi ulibaini kuwa hakuna mikakati ya kutambua maeneo ya kazi ambayo hayajasajiliwa nchini.

(ii) Hakuna rejista ambayo inayoonyesha maeneo ya kazi ya muda mfupi au yaliyofungwa.

(iii) Ubora wa Mipango ya ukaguzi wa usalama na afya mahala pa kazi ni duni na haipangwi kulingana na viashiria vya hatari.

(iv) Adhabu kwa maeneo ya kazi yasiyo sajiliwa hazitekelezwi ipasavyo.

(v) Ukaguzi wa maeneo ya kazi haupangwi kulingana na vihatarishi.

(vi) Hakuna tathmini iliyofanyika ya ubora wa ukaguzi dhidi ya viwango vilivyowekwa. Uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi hautoshelezi.

(vii) Wizara ya Kazi na Ajira haijafanya ufuatiliaji na tathmini juu ya shughuli za usalama na afya mahali pa kazi zinazofanywa na OSHA.

7.2.3 **Mapendekezo ya ukaguzi**

(i) Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) itekeleze ipasavyo wajibu wake kulingana na Sheria ili kuhakikisha uwepo wa mazingira salama mahali pa kazi.

(ii) Wizara ya Kazi na Ajira ihakikishe inafuatilia na kutathmini shughuli za OSHA ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kuweza kuyasajili na kuyakagua maeneo ya kazi ili kuwahakikishia wafanyakazi usalama wao wakiwa mahali pa kazi.

7.3 USIMAMIZI WA MIKATABA YA MIRADI YA UJENZI KATIKA SERIKALI ZA MITAA

7.3.1 Uchunguzi uliofanyika

Ukaguzi ulichunguza kama Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Sekretarieti za Mikoa zina mfumo madhubuti wa kusimamia mikataba ya miradi ya ujenzi katika Serikali za Mitaa ili kupunguza ucheleweshaji, ongezeko la gharama na kasoro za ubora katika miradi ya maendeleo iliyokamilika.

7.3.2 **Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi:**

(i) Makadirio ya muda na gharama za kukamilisha miradi ya ujenzi si ya uhalisia.

(ii) Ukosefu wa utaratibu wa kuhakikisha ubora wa kazi katika hatua za maandalizi ya miradi;

(iii) Kuchelewa kukamilisha miradi;

(iv) Serikali za Halmashauri za Mitaa hazipangilii ipasavyo manunuzi ya makandarasi.

(v) Kuna idadi kubwa ya Miradi iliyopangwa kutekelezwa ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa na Serikali.

(vi) Miradi ya Ujenzi haigharimiwi ipasavyo na Serikali kuu kulingana na Bajeti iliyopitishwa; na

(vii) Kuna udhaifu katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi mbalimbali inayofanywa na Halmashauri.

7.3.3 Mapendekezo ya ukaguzi

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inapaswa kuhakikisha kwamba inafuatilia na kutathmini ipasavyo mipango na utekelezaji wa mikataba ya ujenzi katika miradi ya maendeleo ya Halmashauri.

(ii) Sekretarieti za Mikoa na Wizara husika zitoe misaada ya kutosha wakati wa kupanga na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Halmashauri.

(iii) Halmashauri zinatakiwa kuzingatia ushauri wa wataalamu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha usanifu wa miradi ya ujenzi unafanyika kiufanisi ili kufikia mahitaji ya walengwa.

7.4 USIMAMIZI WA MANUNUZI YA VIFAA VYA TEHAMA KATIKA SEKTA YA UMMA

7.4.1 Uchunguzi uliofanyika

Ukaguzi ulitathmini kiwango ambacho Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia zimesimamia na kutathmini manunuzi ya vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma na iwapo hatua sahihi zimechukuliwa ili kuboresha namna ambavyo mfumo wa manunuzi unafanya kazi. Ukaguzi ulilenga Serikali Kuu na hasa Wizara 4 (nne) ambazo ni Wizara ya Maji, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Viwanda na Biashara

7.4.2 Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi:

(i) Ukadiriaji wa mahitaji ya vifaa vya TEHAMA katika sekta ya umma haufanyiki kwa kuzingatia mahitaji halisi.

(ii) Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia haijaandaa miongozo na viwango vinavyotakiwa katika ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na kuratibu utekelezaji wake.

(iii) Wanunuzi (Procuring Entities) hawafuati viwango vya ukomo wa bei vilivyowekwa na wakala wa manunuzi (GPSA);

(iv) Vifaa vya TEHAMA vilivyowasilishwa havikufanyiwa ukaguzi kikamilifu;

(v) Wanunuzi hawajitathmini na hawatathmini utendaji wa maafisa ugavi.

(vi) Divisheni ya Sera ya Manunuzi ya Umma (PPD) imeshindwa kuandaa Sera ya Manunuzi ya Taifa na Viwango vya manunuzi kwa vyombo vya serikali ingawa kiasi cha fedha kilichotolewa kwa shughuli hiyo kilikwishatumiwa.

(vii) Divisheni ya Sera ya Manunuzi ya Umma (PPD) haijawahi kufuatilia na kutathmini mfumo wa manunuzi katika wizara, Idara na wakala wa serikali (MDAs).

Ukaguzi ulihitimisha kuwa Wizara ya Fedha kupitia Divisheni ya Sera ya Manunuzi ya Umma (PPD) haijatoa kipaumbele katika ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa manunuzi katika miaka mitatu iliyopita.

7.4.3 Mapendekezo ya ukaguzi

(i) Wizara ya Fedha kupitia Divisheni ya Sera ya Manunuzi ya Umma (PPD) inatakiwa kufuatilia na kutathmini ipasavyo manunuzi yanayofanyika katika Taasisi za Umma.

(ii) Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ihakikishe kunakuwepo na udhibiti na uratibu mzuri wa viwango vya

ubora wa vifaa vya TEHAMA ili kuleta tija katika matumizi ya vifaa hivyo.

(iii) Wanunuzi wazingatie miongozo mbalimbali inayotolewa na Wizara zenye dhamana katika TEHAMA na manunuzi ya umma.

7.5 USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA ZIWA VICTORIA

7.5.1 Uchunguzi uliofanyika

Ukaguzi ulichunguza kama Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imefuatilia na kutathmini ipasavyo shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria ili kukabiliana na tatizo la uvuvi wa sangara uliopita viwango (Overfishing). Ukaguzi ulitumia taarifa za kipindi cha miaka mitatu kuanzia Juni, 2008 hadi Desemba, 2011. Pia taarifa zilikusanywa kutoka wilaya 15 zenye shughuli za uvuvi katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Waziri Mkuu zina wajibu wa kuandaa, kutekeleza, kufuatilia (monitoring) na kupitia marekebisho ya muundo wa sera na kanuni za uvuvi nchini Tanzania.

7.5.2 Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi:

(i) Kiasi cha samaki kinachokadiriwa kubaki ziwani kipo chini kupita kiasi kilichopendekezwa. Kiwango kinachotakiwa kwa Tanzania ni tani 382,500

lakini kiwango kilichopo kinakadiriwa kuwa tani 165,000.

(ii) Asilimia 50 ya wavuvi na vyombo vya uvuvi katika Ziwa Victoria havijasajiliwa.

(iii) Kuna ufuatiliaji hafifu wa shughuli za uvuvi ziwani.

(iv) Vikundi vya usimamizi wa mialo (Beach Management Units) vina uwezo mdogo katika kuzuia uvuvi haramu.

(v) Taarifa za uvuvi hazifuatiliwi vya kutosha ili kuhakikisha kwamba takwimu sahihi zinakusanywa.

(vi) Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na uvuvi haramu usioripotiwa na kudhibitiwa hazitoshelezi.

7.5.3 **Mapendekezo ya ukaguzi**

(i) Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ihakikishe kwamba inadhibiti ipasavyo uvuvi katika Ziwa Victoria ili kunusuru kutoweka kwa samaki aina ya sangara. Hii ni pamoja na kufuatilia na kutathmini shughuli za uvuvi na kuhakikisha kwamba utendaji wa sekta ya uvuvi unaratibiwa na kutathminiwa ipasavyo.

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana zinapaswa kuhakikisha kwamba zinafuatilia na kutathmini ipasavyo shughuli za uvuvi kwenye Halmashauri. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba Halmashauri zinaratibu na kufadhili shughuli zinazofanywa na Vikundi vya usimamizi wa mialo ili kuongeza tija na ufanisi.

7.5.4 **Hitimisho la jumla**

Mambo yaliyojadiliwa katika ripoti hii yanahitaji kutazamwa na kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Wizara, Idara, Taasisi, Wakala, Shirika na Halmashauri. Baadhi ya malengo yaliyopangwa na Serikali yanaweza kuwa ni vigumu kufikiwa kutokana na mapungufu yaliyobainishwa katika ukaguzi. Natoa wito kwa serikali kufanyia kazi mapungufu yote yaliyojitokeza kwenye ukaguzi wetu ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji wa Serikali na hivyo kufanikiwa kutoa huduma bora zaidi kwa umma.

UJUMBE KWA WADAU WOTE WA RIPOTI HII

SURA YA NANE

8.0 UJUMBE KWA WADAU WOTE WA RIPOTI HII

(i) Serikali

Pamoja na Serikali kuonyesha jitihada za kutekeleza mapendekezo mbalimbali yanayotolewa na Ofisi yangu, ni dhahiri kuwa jitihada zaidi zinahitajika kufanyika ili mapendekezo yote yaliyotolewa yatekelezwe kwa wakati. Hulka na tabia ya kutotekeleza mapendekezo yangu inapelekea kujirudia rudia kwa hoja ambazo zimetolewa na wakaguzi kwa miaka ya nyuma na hii inaashiria kuwepo kwa mapungufu katika uwajibikaji Serikalini. Ningependa kuifahamisha Serikali kwamba mapendekezo ninayoyatoa yana lengo la kuhakikisha uwepo wa umakini katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, uangalizi, utoaji na matumizi mazuri ya Mali za Umma. Mapendekezo hayo pia yanalenga kuhakisha matumizi ya Fedha za Umma yanaidhinishwa na wenye madaraka husika na fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuhakikisha tija na ufanisi katika kutumia rasilimali za Taifa kwa kuzingatia Sheria.

Ni matumaini yangu kuwa utekelezaji huo utasaidia kuleta maendeleo na kuboresha zaidi utendaji wa Serikali ili kuongeza thamani ya huduma zitolewazo kwa Umma.

(ii) Bunge Kupitia Kamati zake mbalimbali

Kutokana na Bunge kuwa chombo kikuu cha kuisimamia Serikali kupitia Kamati zake mbalimbali, ni matumaini yangu kuwa Kamati zitafanya kazi kwa nia ya dhati kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza kwa wakati mapendekezo yote yanayotolewa na ofisi yangu ili kuwaletea Wananchi maendeleo na kuongeza tija katika huduma zitolewazo na Serikali kwa jamii.

(iii) Umma wa Tanzania

Ili kuendeleza dhana ya Uwazi na Uwajibikaji na kuwawezesha wananchi wengi kupata taarifa za matokeo ya kaguzi zinazofanywa na ofisi yangu, kwa mara ya kwanza nimetoa ripoti hii inayojumuisha muhtasari wa ripoti zote nilizowasilisha kwa Mheshiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni haki ya Kikatiba kwa kila mwananchi kupashwa habari na taarifa sahihi, kwa dhana hiyo nimeona ni vyema kutoa kitabu hiki kitakachoweza kutumiwa na kusomwa na wananchi wengi zaidi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa ripoti hii itawapa fursa wananchi kufahamu mambo mbalimbali yanayoripotiwa na ofisi yangu kupitia ripoti jumuisho za ukaguzi za kila mwaka.

(iv) Wafadhili

Napenda kutoa Shukrani za dhati kwa Wafadhili mbalimbali wanaoisaidia ofisi yangu kwa misaada ya kifedha na vitendea kazi ili kuendana na Teknolojia za kisasa na pia kufanya ukaguzi kwa njia za kisasa zaidi. Ni matarajio yangu kuwa tutaendelea kushirikiana na Wafadhili ili kuhakikisha kuwa ofisi yangu inaimarika na inachangia katika kuwaletea maendeleo Wananchi kwa kutoa mapendekezo yenye tija na ambayo yakitekelezwa na Serikali wananchi watafaidika kwa kiwango kikubwa.

Kwa taarifa zaidi za ukaguzi wa hesabu za serikali tembelea tovuti yetu

www.nao.go.tz

Dira

" Kuwa kituo cha ubora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya umma"

Dhima

"Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma"

Kwa Mawasiliano,

Barabara ya Samora / Mtaa wa Ohio

S.L.P. 9080, Dar es Salaam - Tanzania

Simu: + 255 22 2115157 / 8

Nukushi: + 255 22 2117527

Baruapepe: ocag@nao.go.tz

Tovuti: www.nao.go.tz